HOTUBA YA MGENI RASMI MHESHIMIWA ZELOTE STEPHEN ZELOTE ALIPOFUNGUA MAFUNZO YA MWONGOZO KWA WAHESHIMIWA MADIWANI KWA AJILI YA KUWAJENGEA UWEZO WAKATI WA KUPITIA TAARIFA ZA FEDHA NA KUFANYA TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA PROGRAMU YA MABORESHO YA USIMAMIZI WA FEDHA KATIKA SEKTA YA UMMA AWAMU YA NNE YALIYOFANYIKA TAREHE 17 MEI, 2017

Ndugu Katibu Tawala wa Mkoa,

Mheshimiwa Meya wa Manispaa ya Sumbawanga,

Waheshimiwa Wenyeviti wa Halmashauri za Wilaya ya Sumbawanga, Kalambo na Nkasi,

Waheshimiwa Madiwani na Watendaji wote,

Mabibi na Mabwana

Tuna kila sababu kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehema aliyetukutanisha hapa leo tukiwa wenye Afya njema na hasa kwa ajili ya mafunzo haya muhimu ya kuwajengea uelewa Waheshimiwa Madiwani. Ni imani yangu kwamba mafunzo haya yatakuwa chachu na nguzo kuwaletea maendeleo wananchi mnao wawakilisha katika maeneo yenu.

Nawashukuru pia waandaji wa Mafunzo haya pamoja na ninyi waheshimiwa Madiwani kwa heshima ambayo mmenipa niweze kufungua Mafunzo haya. Mafunzo haya ni sehemu ya Juhudi za Serikali kuhakikisha kwamba Mamlaka za Serikali za Mitaa zinajengewa uwezo katika kutekeleza Majukumu yake.

Nichukue fursa hii pia kuwashukuru wadau wetu wa Maendeleo ambao ndio Wafadhili wa Mradi huu kwa ujumla wao wamefanya Mkoa wa Rukwa kuwa miongoni mwa Mikoa 10 inayonufaika kupitia Mradi huu ukilenga zaidi kuboresha mifumo ya Kifedha na Udhibiti wake.

Waheshimiwa Madiwani,

Programu hii imetuhusu kutokana na uwepo wa uwezo Mdogo wa Halmashauri zetu kukusanya Mapato ya Ndani. Ni Matumaini yangu kwamba mtapata uzoefu zaidi kuhusu namna ya uendeshaji wa shughuli za Mamlaka za Serikali za Mitaa. Hii ni pamoja na Mikakati ya kupanua wigo na kuongeza Mapato ya Ndani ya Halmashauri.

Vile vile nimeambiwa kwamba kupitia Programu hii ya Maboresho ya Usimamaizi wa Fedha katika Sekta za

Umma mmepata mafunzo mbalimbali yaliyolenga kuwajengea uelewa katika kusimamia utekelezaji wa Majukumu ya Halmashauri zenu hasa katika eneo la Fedha. Mafunzo hayo ni pamoja na:-

(i) Uainishaji wa Fedha zinazopelekwa ngazi ya chini katika Halmashauri na Vigezo vinavyotumika,

(ii) Matumizi ya Mifumo ya Kodi ya Kielektroniki, Kusimamia Mifumo ya Kodi na Kuweka Data kwenye Mifumo hiyo,

(iii) Maeneo ya Usimamizi wa Fedha na kutoa Taarifa za Fedha na udhibiti wa Mfumo, Mikopo, Uwekezaji na Bajeti,

(iv) Kufanya mapitio ya kina ya Taarifa za Fedha na Utunzaji wa kumbukumbu za Fedha kwenye Serikali za Mitaa,

(v) Usimamizi wa Sheria za Manunuzi na Miongozo ya Manunuzi,

(vi) Upekuzi na uchambuzi yakinifu wa Taarifa za Ukaguzi na Usimamizi wa Mapendekezo ya Ukaguzi.

Mafunzo hayo yote pamoja na haya mtakayopata leo yanalenga kuwaimarisha katika yale mnayoyasimamia hasa katika eneo hili muhimu la usimamizi wa Fedha za Halmashauri. Sina shaka mnafahamu hili ni jukumu la tatu kati ya majukumu sita mliyonayo.

Waheshimiwa Madiwani,

Diwani hushiriki kikamilifu katika Mchakato wa Utekelezaji wa Bajeti na Usimamizi wa Fedha za Halmashauri hasa katika eneo la ufuatiliaji na matumizi kupitia wataalamu kwa kuzingatia mfumo uliopo. Hapa ni muhimu nisisitize kuweka mbele maslahi ya wananchi na kuweka kando maslahi binafsi au kula njama na watendaji wasio waadilifu katika Halmashauri.

Kimsingi napenda kusisitiza kwenu yafuatayo:-

Kwanza**,** kuhakikisha kuwa wataalamu wanatekeleza mipango na kutumia fedha kwa malengo yaliyokusudiwa.

Pili, Ushirikishwaji wa walengwa kwa maana ya wananchi mnaowawakilisha katika mipango yote. Hii ni pamoja na kuwahamasisha kuunga mkono juhudi za

Serikali kujiletea maendeleo. Nitashangaa kusikia Mheshimiwa Diwani kuwazuia watu waliomchagua wasishiriki kwenye mipango ya maendeleo katika Kata yake. Atakuwa hatimizi majukumu yake sita.

Tatu, Uwazi. Mambo yote yaweke hadharani kama ni miradi iwekwe kwenye mbao za matangazo nje na thamani yake.

Waheshimiwa Madiwani,

Kumekuwepo na kasoro nyingi kwenye Miradi ya Maendeleo. Baadhi yake ikiwa ni pamoja na:-

(i) Kuibua Miradi mingi isiyo na kipaumbele au tija kwa wakati mmoja na yote kudorora kwa wakati mmoja.

(ii) Hampati takwimu kikamilifu ya miradi yenu. Hili ni jambo la muhimu na lazima Wakurugenzi walitekeleze.

(iii) Ninyi mnatumika kupitisha mipango ya miradi bila kujiridhisha na yale yaliyoandaliwa na wataalamu wenu.

(iv) Miradi haisimamiwi kikamilifu katika maeneo mnayoyawakilisha mpaka itokee Mkuu wa

Wilaya au Mkoa abaini na kuunda kamati ya uchunguzi ambapo huongeza hasara kwa gharama zake.

(v) Mnakubali kuitumika kwenye mabaraza ya Halmashauri zenu kuidhinisha fedha za miradi kufanya kazi nyingine ambayo haikupangwa.

(vi) Miradi kuwa chini ya viwango.

(vii) Miradi kutokamilishwa kwa wakati.

(viii) Kufanyika malipo kabla kazi haijakamilika

Waheshimiwa Madiwani,

Naamini sasa mnao ufahamu wa kutosha kuhusu umuhimu wa halmashauri zenu kuhakikisha kwamba zinakusanya mapato kwa kiwango cha juu.

Maelekezo ya serikali ni matumizi ya mashine za kielektroniki katika Halmashauri na kuondokana na risiti za kuandika kwa mkono ambazo zilitawala kudhoofisha ukusanyaji wa mapato.

Takwimu zinaonesha hadi kufikia Machi, 2017 idadi ya Mashine zilizokuwa zimenunuliwa ilikuwa ni mashine 140 wakati Mkoa una Mahitaji ya Mashine 438. Bado

tuna upungufu wa Mashine 298. Mwisho wa Wakurugenzi kutekeleza agizo hilo ilikuwa tarehe 30 Machi, 2017 yeyote ambaye hakutii agizo hilo atawajibishwa.

Nitoe wito kwenu Waheshimiwa Madiwani kusimamia kwa karibu sana suala hili na kuhakikisha kila eneo la ukusanyaji wa Mapato linakuwa na Mashine hizi ili kuweza kupunguza/kuondoa mianya ya upotevu wa Mapato katika Halmashauri zetu.

Mwaka huu wa 2016/2017 makusanyo ya Mapato ya Ndani ya Halmashauri hadi kufikia Aprili, 2017 yamefikia asilimia 53.6 tu. Makusanyo haya bado ni kidogo. Simamieni Halmashauri zenu ili makisio yaliyowekwa yaweze kukusanywa kama ilivyokisiwa. Lengo ni kuona hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2017 kila Halmashauri inakusanya mapato yake kwa asilimia 100.

Waheshimiwa Madiwani,

Dhamira ya Serikali ni kuona wananchi wanapata huduma inayostahili hasa wananchi wa hali ya chini kabisa. Kwa kuwa mnalo jukumu la kusimamia fedha

za halmsahuri mnapaswa kuwa makini sana kwa sasa kwa kuwa Serikali itakuwa inafikisha fedha moja kwa moja kwenye ngazi mlipo.

Waheshimiwa Madiwani,

Sasa nawatakia Mafunzo mema. Naamini mtakuwa wasikivu na kuzingatia mada zitakazotolewa.

Baada ya Maelezo hayo, natamka kwamba Mafunzo ya Waheshimiwa Madiwani kuhusu **MWONGOZO WA KUPITIA TAARIFA ZA FEDHA NA TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA PROGRAMU YA MABORESHO YA USIMAMIZI WA FEDHA KATIKA SEKTA YA UMMA AWAMU YA NNE** yamefunguliwa rasmi.

Asanteni kwa kunisikiliza

Zelote Stephen Zelote
MKUU WA MKOA WA RUKWA